**SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR KWA AJILI YA UNUNUZI, UTENGENEZAJI, UHIFADHI NA USAMBAZAJI WA DAWA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**KUANZISHWA KWA WAKALA**

4. Kuanzishwa kwa Wakala.
5. Muhuri na nembo ya Wakala.
6. Malengo ya Wakala.
7. Kazi za Wakala.
8. Uwezo wa Wakala.

**SEHEMU YA TATU**
**USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA WAKALA**

9. Uanzishwaji na muundo wa Bodi.
10. Sifa za Mwenyekiti.
11. Katibu wa Bodi.
12. Kazi za Bodi.
13. Uwezo wa Bodi.
14. Mwenendo wa vikao vya Bodi
15. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

16. Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

17. Idara, Vitengo na Divisheni za Wakala.

18. Wafanyakazi wa Wakala.

## SEHEMU YA NNE
## UNUNUZI, UTENGENEZAJI, UHIFADHI NA USAMBAZAJI WA DAWA

19. Ununuzi wa dawa.

20. Utengenezaji wa dawa.

21 Bohari za Dawa.

22. Uhifadhi wa Dawa.

23. Uhifadhi wa dawa za taasisi binafsi.

24. Usambazaji wa dawa.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

25. Vyanzo vya fedha za Wakala.

26. Bajeti ya Wakala.

27. Kufungua akaunti ya Benki

28. Hesabu na ukaguzi.

29. Ripoti ya Mwaka ya Wakala.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

30. Usambazaji na ukusanyaji wa dawa kimakosa.

31. Uangamizaji wa dawa zisizofaa.

32. Maadili kwa Maafisa wa Wakala.

33. Usajili wa wapewa huduma.

34. Kanuni.

## JADWELI

**SHERIA NAM. 12 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

..........1 Februari.........., **2024**

# SHERIA YA KUANZISHA WAKALA WA BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR KWA AJILI YA UNUNUZI, UTENGENEZAJI, UHIFADHI NA USAMBAZAJI WA DAWA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar ya 2023 na itaanza kutumika baada ya kusainiwa na Rais.

Matumizi.

**2**. Sheria hii itatumika kwa mambo yote yanayohusiana na ununuzi, utengenezaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa kwa vituo vya afya vya umma na binafsi ambavyo vinaweza kuhitaji huduma ya Wakala.

Ufafanuzi.

**3**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yanahitaji vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala iliyoanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 9(1) cha Sheria hii;

"Bohari" maana yake ni ghala ya dawa au sehemu maalumu iliyowekwa kwa ajiii ya kuhifadhia dawa kabla ya kusambazwa au kupelekwa sehemu nyengine;

“Dawa” maana yake ni kitu chochote au mchanganyiko wa vitu vilivyotengenezwa, vilivyouzwa au vilivyotolewa kwa ajili ya matumizi katika;

(a) utambuzi, matibabu, kupunguza au kuzuia ugonjwa, hali isiyo ya kawaida ya mwili au akili au dalili zake kwa binaadamu au mnyama;

(b) kurejesha, kurekebisha au urekebishaji wa manufaa kwa manufaa ya kazi ya mwili au akili kwa binaadamu au mnyama;

(c) kuuwa vijidudu katika majengo ambayo dawa zinatengenezwa, zinatayarishwa au zinahifadhiwa, hospitali, vifaa na maeneo ya kilimo; au

(d) vifaa vinavyokusudiwa kutumika kama sehemu ya vifaa vyovyote vilivyoainishwa katika aya ya (a), (b) au (c) na pia inajumuisha vifaa vya matibabu au sehemu ya vifaa hivyo au viambatanisho vyake;

“Dawa zisizofaa” maana yake ni dawa ambazo hazifai kwa matumizi ya binaadamu au mnyama kutokana na kumalizika muda wake wa matumizi, kutofanya kazi au matumizi yake yamesitishwa na mamlaka inayohusika;

“Kifaa tiba” maana yake ni chombo, kifaa bandia, zana, kifaa cha matibabu, mashine, kipandikizi, kitendanishi cha ndani ya mwili au vifaa vyengine vinavyofanana au vinavyohusiana, ikijumuisha kipengele chochote, sehemu au nyongeza;

“Kituo cha afya” maana yake ni taasisi yoyote kwa ajili ya mapokezi na matibabu ya watu waliojeruhiwa, dhaifu au wanaosumbuliwa na maradhi, na inajumuisha hospitali, kituo cha afya, zahanati, nyumba ya uzazi, kliniki (iwe inahama au vyenginevyo) na pia mahali au majengo yoyote yanayotumika kwa madhumuni ya matibabu, iwe ya kikawaida au kwa muda.

“Mkurugenzi Mkuu” maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria hii;

“Mpewa huduma” maana yake ni kituo cha afya, taasisi au mtu yeyote anayepokea huduma kutoka kwa Wakala;

“Rais” maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Wakala" maana yake ni Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar ulioanzishwa chini ya kifungu cha 4(1) cha Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na afya.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA WAKALA

Kuanzishwa kwa Wakala.

**4**.-(1) Kunaanzishwa Wakala utakaojulikana kama Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar.

(2) Wakala kwa kuzingatia sheria, utakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki au kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(d) kukopa kiasi chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya fedha; na

(e) kufanya kitendo chochote ambacho Wakala kwa asili yake kisheria, unastahili kukifanya.

Muhuri na nembo ya Wakala.

5.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Wakala katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Wakala katika nyaraka yoyote itathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mkuu au Afisa aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Nyaraka yoyote inayokusudiwa kuwa ni hati iliyotolewa na Wakala, uliyotiwa muhuri wa Wakala na kuthibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, itachukuliwa kuwa ni hati ya Wakala.

Malengo ya Wakala.

6. Wakala utakuwa na malengo ya:

(a) kusimamia masuala yote yanayohusiana na ununuzi, utengenezaji, uhifadhi, usambazaji na uuzaji wa dawa unaofanywa na Wakala; na

(b) kuhakikisha upatikanaji endelevu wa dawa zenye ubora kwa bei nafuu.

Kazi za Wakala.

7.-(1) Wakala utakuwa na kazi ya:

(a) kuuza, kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa kwa mpewa huduma;

(b) kutengeneza au kushirikiana na kampuni za kutengeneza dawa wakati wa kutengeneza dawa;

(c) kuhakiki na kudhibiti ubora na usalama wa dawa wakati wa ununuzi, utengenezaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa kwa mpewa huduma bila ya kuathiri sheria nyengine yoyote;

(d) kuendeleza, kutunza na kusimamia mfumo wa manunuzi, uhifadhi na usambazaji wa dawa zilizoidhinishwa zinazohitajika kwa ajili ya matumizi ya mpewa huduma wenye ufanisi na wa gharama nafuu;

(e) kutumia misingi madhubuti ya kibiashara ambayo inatumika katika ununuzi, uhifadhi na usambazaji wa dawa ili kudhibiti mfuko unaojiendesha kwa ajili ya uendeshaji wa Wakala;

(f) kuainisha mahitaji ya dawa zinazohitajika nchini;

(g) kupanga bei za dawa zinazosambazwa na Wakala;

(h) kusajili na kutunza kumbukumbu za mpewa huduma;

(i) kufanya utafiti unaohusiana na kazi za Wakala;

(j) kushirikiana na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa katika utekelezaji wa mkakati endelevu wa upatikanaji wa dawa;

(k) kushirikiana na sekta binafsi katika kutengeneza, kununua, kusambaza, kuhifadhi, kudhibiti na kufanya utafiti wa dawa; na

(l) kufanya kazi nyengine yoyote iliyopewa chini ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri kazi zilizoelezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Wakala unaweza kupokea msaada wowote wa dawa uliotolewa kwa Serikali.

(3) Wakala unaweza, baada ya idhini ya Bodi, kuingia katika makubaliano na taasisi yoyote yenye maslahi sawa kwa ajili ya kuboresha ufanisi wake na ubora wa huduma kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Uwezo wa Wakala.

**8**. Katika kutekeleza kazi zake, Wakala utakuwa na uwezo wa:

(a) kuzuia usambazaji wa dawa kwa kituo cha afya ambacho kinakiuka miongozo ya usambazaji na uhifadhi wa dawa;

(b) kuhitaji taarifa kutoka kwa mpewa huduma ili kutambua kiwango cha dawa kinachohitajika kununuliwa;

(c) kukataa kupokea dawa ambazo hazikidhi viwango vilivyowekwa na mamlaka husika; na

(d) kutekeleza uwezo wowote uliopewa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TATU
## USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA WAKALA

Uanzishwaji na muundo wa Bodi.

9.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala ambayo itaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Mfamasia Mkuu wa Serikali;

(d) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(e) mwakilishi kutoka hospitali ya rufaa ya mwisho;

(f) mtaalamu wa dawa kutoka sekta binafsi; na

(g) mtaalamu wa fedha kutoka Wizara inayohusika na Fedha.

(2) Isipokuwa kwa Mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine wa Bodi waliotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) (d), (e), (f) na (g) watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, taaluma na usawa wa kijinsia.

Sifa za Mwenyekiti.

**10**. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sayansi ya afya kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika masuala yanayohusiana na sayansi za afya;

(c) ana umahiri katika kusimamia masuala ya taasisi kwa ufanisi na ubora; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

**11**.-(1) Bodi itamteua mfanyakazi wa Wakala kuwa Katibu wa Bodi

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo:

(a) ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria kutoka taasisi inayotambuliwa na Serikali au kuwa na sifa ya kuwa katibu wa shirika; na

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu katika utumishi wa umma;

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na:

(a) kwa kushauriana na Mwenyekiti, ataandaa ajenda za vikao vya Bodi;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za vikao vya Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(e) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyopangiwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

**12.** Bodi itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia uendeshaji wa Wakala;

(b) kumshauri Waziri kuhusu maendeleo ya sera na mikakati yanayohusiana na huduma zinazotolewa na Wakala;

(c) kupitia na kuidhinisha sera, mpango wa biashara na uendeshaji, bajeti, ripoti na taarifa za ukaguzi wa fedha za Wakala;

(d) kutoa muongozo wa kimkakati;

(e) kuhakikisha utawala bora, sera na utendaji ulio bora upo na unatekelezwa;

(f) kuhakikisha ufanisi wa matumizi ya rasilimali za Wakala; na

(g) kutekeleza kazi nyengine yoyote iliyoainishwa katika Sheria hii.

Uwezo wa Bodi.

**13**. Bodi itakuwa na uwezo wa jumla wa usimamizi unaohusiana na utekelezaji wa kazi za Wakala, na mahsusi itakuwa na uwezo wa:

(a) kuanzisha Kanuni za Wafanyakazi na Kanuni za Usimamizi wa Fedha kwa ajili ya Wakala;

(b) kupendekeza muundo wa utumishi wa Wakala;

(c) kupendekeza kwa mamlaka husika, mabadiliko yoyote ya mishahara, maposho au vigezo na masharti mengine ya utumishi ya wafanyakazi wa Wakala;

(d) kuidhinisha ada, viwango na tozo nyengine zinazohusiana na huduma zinazotolewa na Wakala;

(e) kuajiri na kuteuwa wafanyakazi wa Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011; na

(f) kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mfanyakazi yeyote kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

Mwenendo wa vikao vya Bodi.

**14**.-(1) Masharti kuhusiana na mwenendo wa vikao vya Bodi yatakuwa kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

(2) Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti, kurekebisha Jadweli chini ya masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

**15**.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Wakala ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sayansi ya dawa, mnyororo wa ugavi, ununuzi, usimamizi wa biashara au fani nyengine yoyote inayolingana na hizo kutoka taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi katika fani yoyote iliyoainishwa katika aya (a) kwa kipindi kisichopungua miaka mitano; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

**16**.-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala na atakuwa na wajibu wa kusimamia kazi za kila siku za Wakala.

(2) Katika kutekeleza kazi zake, Mkurugenzi Mkuu atakuwa na jukumu la:

(a) kuwa na dhamana ya mapato na matumizi ya Wakala;

(b) usimamizi mzuri wa fedha na mali za Wakala;

(c) utekelezaji wa mpango mkakati, mpango wa biashara na mpango wa uendeshaji wa Wakala;

(d) kusimamia masuala ya Wakala katika utoaji wa huduma bora na wenye ufanisi;

(e) kuwa kama mshauri mkuu wa Serikali katika masuala yote yanayohusiana na ununuzi, utengenezaji, uhifadhi na usambazaji wa dawa kwa ajili ya vituo vya afya vya umma;

(f) kuhakikisha matumizi bora ya wafanyakazi na rasilimali nyengine za Wakala;

(g) kutunza daftari la kumbukumbu la wapewa huduma wa Wakala;

(h) kutekeleza sera za kitaifa zinazohusiana na dawa; na

(i) kutekeleza majukumu mengine yoyote kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Idara, Vitengo na Divisheni za Wakala.

**17**.-(1) Wakala unaweza kuanzisha idara, vitengo na divisheni kama itakavyoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Bodi kutokana na mapendekezo ya Mkurugenzi Mkuu ambao watakuwa ni watu wenye ujuzi unaohusika na uzoefu wa kutosha kufanya kazi katika idara na vitengo vyao husika na watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kulingana na sifa na uzoefu wao na watawajibika kwa wakuu wa idara zao husika.

Wafanyakazi wa Wakala.

**18**. Wakala unaweza, kwa kuzingatia vigezo na masharti, kuajiri wafanyakazi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

## SEHEMU YA NNE
## UNUNUZI, UTENGENEZAJI, UHIFADHI NA USAMBAZAJI WA DAWA

Ununuzi wa dawa.

**19**. Wakala utanunua dawa kwa kufuata masharti ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016.

Utengenezaji wa dawa.

**20**.-(1) Wakala utatengeneza dawa kwa kufuata Miongozo mizuri ya Utengenezaji Dawa iliyowekwa na mamlaka husika.

(2) Wakala, katika kutengeneza dawa, utazingatia aina za dawa zinazotumika au zinazohitajika kwa wingi na zenye gharama nafuu.

Bohari za Dawa.

**21**.-(1) Kutakuwa na Bohari za Dawa ambazo zitamilikiwa na Wakala na zitatumika kwa ajili ya kuhifadhia dawa.

(2) Wakala unaweza kuanzisha bohari nyengine za dawa katika eneo jengine lolote endapo itakuwa ni muhimu.

Uhifadhi wa Dawa.

**22**.-(1) Wakala utakuwa na wajibu wa kuhifadhi dawa zilizonunuliwa na Wakala, zilizopatikana kwa njia nyengine yoyote au zinazomilikiwa na taasisi za umma au binafsi.

(2) Uhifadhi wa dawa utazingatia miongozo kwa ajili ya utunzaji sahihi wa dawa itakayotolewa na Wakala.

(3) Wakala utahifadhi dawa katika bohari zake au bohari nyengine zinazotambuliwa na Wakala.

Uhifadhi wa dawa za taasisi binafsi.

**23**. Wakala unaweza kuhifadhi dawa za taasisi binafsi kwa utaratibu maalum na kwa kuzingatia kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Usambazaji wa dawa.

**24**.-(1) Wakala utasambaza dawa kwa mujibu mahitaji ya mpewa huduma.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, Wakala unaweza kutumia taasisi yoyote kusambaza dawa.

(3) Usambazaji wa dawa kwa mpewa huduma yeyote utafanywa baada ya mpewa huduma kutimiza taratibu kama ilivyoainishwa katika kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha za Wakala.

**25**.-(1) Fedha na rasilimali za Wakala zitajumuisha:

(a) fedha zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) ada au tozo zinazolipwa kwa Wakala kutokana na utoaji wa huduma zake;

(c) ruzuku, zawadi, misaada, michango, mikopo, urithi au uwekezaji halali unaoweza kupokelewa kutoka kwa mtu au taasisi yoyote; na

(d) fedha nyengine zozote ambazo zinaweza kupokelewa au kupatikana kisheria na Wakala iwe katika shughuli zake au vyenginevyo.

(2) Miamala yote ya fedha ya Wakala itafanywa na kusimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

(3) Wakala utabakiza asilimia fulani ya fedha zitakazokusanywa kutokana na huduma zinazotolewa na Wakala kama itakavyoamuliwa na Waziri anayehusika na Fedha.

Bajeti ya Wakala.

**26**.-(1) Mkurugenzi Mkuu, kwa kila mwaka wa fedha ataandaa na, atawasilisha kwa Bodi kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wakala kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

(2) Baada ya makadirio kujadiliwa na kuidhinishwa, bajeti ya Wakala itachukuliwa kuwa ni sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Wakala yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na miongozo mengine yoyote kama itakavyotolewa na Serikali kila baada ya muda.

(4) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa kwa fedha za Wakala yanafanywa kwa usahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti wa kutosha utadumishwa juu ya mali na madeni ya Wakala

Kufungua akaunti ya Benki

**27**. Wakala utafungua akaunti ya benki kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na kuweka fedha zake kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

Hesabu na ukaguzi.

**28**.-(1) Wakala utaweka na kutunza kwa usahihi vitabu vya hesabu ambavyo vinajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Hesabu zote za Wakala zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016 na sheria nyengine zozote za fedha zinazohusika.

Ripoti ya Mwaka ya Wakala.

**29**. Wakala, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016, utawasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka inayohusiana na mwaka huo itakayojumuisha:

(a) nakala ya hesabu za Wakala zilizokaguliwa pamoja na ripoti ya mkaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) ripoti ya utekelezaji kulingana na shabaha za Wakala na taarifa nyengine yoyote inayohusiana nayo;

(c) ripoti inayohusiana na utendaji wa Wakala kwa kipindi cha mwaka huo wa fedha; na

(d) taarifa nyengine yoyote inayohusiana na kazi za Wakala kama Waziri atakavyohitaji.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI MENGINEYO

Usambazaji na ukusanyaji wa dawa kimakosa.

**30**.-(1) Mpewa huduma atakuwa na jukumu la kuutaarifu Wakala kuhusu usambazaji wa dawa kimakosa uliofanywa na Wakala kwa kuzingatia kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Wakala unaweza kuzikusanya dawa zozote kutoka kwa mpewa huduma ikiwa dawa zilizosambazwa:

(a) zimezidi kiwango kilichoagizwa;

(b) zina dosari;

(c) zimesitishwa matumizi yake na mamlaka husika;

(d) zimemaliza muda wake wa matumizi; au

(e) zimesambazwa kimakosa.

Uangamizaji wa dawa zisizofaa.

**31**. Wakala unaweza kuangamiza dawa zisizofaa kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika sheria husika.

Maadili kwa Maafisa wa Wakala.

**32**. Kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 au sheria nyengine yoyote inayohusiana na kanuni za maadili, Wakala utaweka Miongozo ya utekelezaji wa kazi kwa maofisa wa Wakala.

Usajili wa wapewa huduma.

**33**.-(1) Wakala utasajili wapewa huduma wote kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Wakala utaandaa daftari la kumbukumbu maalumu ambalo litajumuisha taarifa zote muhimu za wapewa huduma.

Kanuni.

**34**.-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni kuhusu:

(a) uagizaji na upokeaji wa dawa;

(b) uhifadhi wa dawa na uwekaji dawa katika Bohari ya Dawa;

(c) usambazaji na ukusanyaji wa dawa; na

(d) ada na tozo zinazotokana na huduma zinazotolewa na Wakala.

## JADWELI

## MWENENDO WA BODI
**[Chini ya kifungu cha 14(1)]**

---

Makamu Mwenyekiti.

**1**. Wajumbe wa Bodi, katika kikao chao cha mwanzo cha Bodi watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**2**. Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

**3**.-(1) Bodi itakutana katika vikao vya kawaida mara moja kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana katika vikao vya dharura muda wowote inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikaò vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

**4**. Akidi katika vikao vyote vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wake.

Uamuzi wa Bodi.

**5**. Uamuzi wa Bodi utafanywa kwa makubaliano, ikiwa hakuna makubaliano, uamuzi utafanywa kwa wingi wa kura na ikitokea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za vikao.

**6**. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuandaa taratibu zake zenyewe kuhusiana na vikao na utaratibu wa kutekeleza shughuli zake ikijumuisha kamati za Bodi.

Mjumbe mualikwa.

**7**. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya vikao vya Bodi kama mtaalamu, lakini mtu aliyealikwa hatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbukumbu za vikao vya Bodi.

**8**. Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

Kubainisha maslahi.

**9**.-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kujadiliwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha maslahi:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya uamuzi; au

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

**10**. Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya kuwa na sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu za afya ya kimwili au kiakili;

(d) kusitishwa na Waziri kwa kushindwa kutimiza matarajio ya Wakala;

(e) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyompendekeza mjumbe huyo; au

(f) kifo.

Kamati za Bodi.

**11**. Bodi inaweza kuunda kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalum kama itakavyoona inafaa.

kukasimu kazi za Bodi.

**12**.-(1) Bodi inaweza, pale itakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa kamati ya Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa kazi hizo.

Posho kwa wajumbe.

**13**. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011 na sheria nyengine zinazohusika.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 6 Disemba, 2023.

.............................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***